



VIELELEZO NA MINA PRICE

Kumfuata Yesu huko Papua New Guinea

Jinsi Erwin Anavyomfuata Yesu

Erwin anamfuata Yesu kwa kuwasaidia wazee katika mji wake. Anasaidia kusafisha ua wao na kuwapelekea chakula. “Nina furaha ninapowasaidia wao. Nataka kusaidia zaidi,” anasema.

Erwin pia humfuata Yesu kwa kusali kwa Baba wa Mbinguni. “Ninaposali, ninahisi kama vile Mungu yupo nami,” anasema.

Erwin alisali kumwomba Baba wa Mbinguni kuisaidia familia yake kuwa pamoja milele. Erwin na familia yake walienda hekaluni huko Tonga kuunganishwa kama familia. Anasema, “Nilimhisi Roho ndani ya hekalu. Kulikuwa na amani sana na ukimya.” ●



Erwin na familia yake wakiwa kwenye Hekalu la Nuku'alofa Tonga.

Wewe Pia Unaweza Kumfuata Yesu!

Ni kipi umefanya ili kumfuata Yesu? Andika na utueleze! Nenda kwenye jalada la nyuma ili kuona jinsi ya kufanya hilo.



Gude



Kuhusu Erwin

UMRI MIAKA: 7

KUTOKA: Mkoa wa Kati, Papua New Guinea

LUGHA: Kiingereza na Kitok Pisini

MALENGO: 1) Kuwa rubani 2) Kuwa mmisionari.

ANAVYOVIPENDA: Kucheza dansi na kuvua samaki

FAMILIA: Mama, Baba, kaka wakubwa watatu na dada mmoja mkubwa

Mambo Ayapendayo Erwin

HADITHI YA KITABU CHA MORMONI: Wakati nafi alipojenga mashua (ona Nefi 17–18.)

DESTURI YA FAMILIA: Kukusanyika kwa familia yote katika kijiji ili kula pamoja

TUNDA: matufaha

RANGI: Nyekundu

WIMBO WA MSINGI: “I Am a Child of God” (*Kitabu cha Nyimbo za Watoto, 2*)